Ndoa ni jambo la kiagano ambalo linahusisha watu wa jinsia mbili tofauti yaani mwanamke na mwanaume,ndoa ni jambo jema ambalo Mungu mwenyewe amelipa kibali tangu mwanzo.Taasisi ya ndoa haikutokana na mahitaji tu ya mwanadamu bali Mungu mwenyewe aliianzisha alipoona upweke ndani ya Adam.

Ni kweli kuwa Adam alikuwa na upweke lakini hilo halikumfanya ashindwe kuishi ,hata kama Mungu asingemletea mke bado Adam angeendelea kuishi lakini katika hekima ya Mungu aliona ni vyema huyu mtu (Adam) apate mwenza ili kusudi wakamilishane katika maisha yao ndipo wazo la ndoa lilipokuja .

Mwanzo 2:18
*"Bwana Mungu akasema ,Si vyema huyu mtu awe peke yake,nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye"*
Maandiko yanasema kuwa Mungu aliona si vyema Adam awe peke yake lakini hayasemi ilikuwa ni lazima Adam asiwe peke yake yaanihapo kuna mambo mawili tofauti kabisa ambayo watu wanayachanganya (Si vyema na ni lazima).

Iko hivi…
Mtu anaweza kusema si vyema wewe kula ugali lakini haimanishi kwamba ni lazima wewe kutokula ugali.Sijui umeelewa hapo?
Inaweza ikawa si vyema wewe kufanya jambo fulani lakini haimaanishi kuwa ni lazima wewe kutokufanya jambo hilo.Kama haujaelewa rudia kusoma tena utaelewa ninachomaanisha.

Kwahivyo Mungu aliona si vyema mtu mume awe peke yake lakini hilo halikumaanisha asingepata mke maisha yake

yangeishia hapo,maisha ya Adam yalikuwepo kabla hata ya kupewa mke na baada ya kupewa mke pia.Point yangu ya msingi hapo ni kwamba NDOA NI NJEMA ILA SIO YA LAZIMA.
Kwanini nasema hivyo?
Soma hapa ……
*“Wanafunzi wake wakamwambia,mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo haifai kuoa “*

*“Lakini yeye akawaambia,si wote wawezao kulipokea neno hili,ila wale waliojaliwa “*

*“Maana wako matowashi waliozaliwa hali hiyo toka matumboni Mwa mama zao,tena wako matowashi waliofanywa na watu kuwa matowashi,tena wako matowashi wanaojifanya kuwa matowashi Kwa ajili ya ufalme wa mbinguni.Awezaye kulipokea neno hili na alipokee”*
Mathayo 19:10-12

Ukisoma andiko hilo kuanzia mstari wa kwanza ndipo utaelewa zaidi Yaan hapo Yesu alikuwa anazungumzia kwa habari ya talaka na akasema Musa aliruhusu kuachana kwasababu ya ugumu wa mioyo ya watu wa kipindi kile lakini Mungu anakuchukia kuachana kwahiyo ikitokea mke na mume wameachana basi sababu kuu iweuasherati / uzinzi na atakaye achika asiolewe na mume asioe kabisa.

Ndipo wanafunzi wakaona mambo ni magumu hivyo wakamwambia si bora basi watu wasioe kama mambo yenyewe ni magumu hivyi , ndipo Yesu akawapa jibu ambalo ndo nataka nikuonyeshe .Akasema “sio wote waliojaaliwa kuweza kustahimili kuto kuoa

ama kutokuolewa lakini wapo wenye uwezo juu ya hilo ambalo ni watumishi wa Mungu/matowashi.

Hii ni kumaanisha kuwa ndoa ni ya muhimu ila sio kwa ajili ya watu wote /sio ya kulazimisha.Ikiwa Yesu mwenyewe ametuambia hapo kuwa wapo watu waliozaliwa ili kuwa hivyo (matowashi wasiooa)

Kwahiyo suala na ndoa lisikupe shida ukahisi usipoolewa umepata dhambi,hapana ni suala ambalo Mungu mwenyewe kupitia Yesu anadhihirisha kuwa sio wote watakaoingia katika agano la ndoa.Lengo langu sio kupinga suala la ndoa il anataka uelewe kuwa ndoa sio ya kulazimisha kwa akili zako unapoona kila kitu kinagoma .
Just relax!!!.

Kuwa singo (kuchelewa kuolewa) sio laana kama watu wengi wanavyochukulia,miaka ya usingo sio miaka iliyolaaniwa dada yangu bali ni miaka Mungu aliyokupa kama zawadi hapa duniani.Najua utanishangaa kwanini nasema hivyo?Usijali utanielewa tu.

Miaka ya usingo sio miaka ya kusubiri Kwa ajili ya ndoa bali ni miaka ya kujiandaa kutengeneza kesho yako unayoitamani kuwa.Miaka ya usingo ndo miaka ya kupambana kujua nini hasa unapaswa kufanya hapa duniani kwasababu hilo ndilo litakupa urahisi wa kujua uolewe na mwanaume wa aina gani.

Watu wengi huchukia kuwa singo na kujiona kama watu wasio na bahati,huu ni mtazamo potofu mno kwenye akili za mabinti na wanawake wengi, ngoja nikupe siri.Hivi unajua kuna wanawake leo wameolewa lakini wanatamani miaka irudi nyuma warudi kuwa singo ili waweze

kukamilisha baadhi ya mambo ya muhimu kuhusu maisha yao?Unafahamu hilo kweli ?

Wapo wanawake wengi leo wamepoteza dira na maana ya maisha mara baada tu ya kuingia kwenye ndoa na wanaume wasiojielewa, ndoto na maono mengi ya mabinti yamekufa kwasababu tu ya kitu kinachoitwa ndoa,kwahiyo nataka utambue kuwa ndoa sio kila kitu bali jambo la msingi kuliko yote ni wewe kuanza kupambania kuishi kusudi la maisha yako sasa ukiwa bado uko singo .

Dada yangu,ukiwa bado singo unakuwa na uhuru mkubwa wa kimaamuzi tofauti na ukishaolewa ndo maana nakwambia furahia sana miaka yako ya usingo.Ndio maana Paulo akasema hivi..
"*Mwanamke aliyeolewa hujishughulisha sana na namna atakavyompendeza mumewe*"
1Wakorinto 7:34

Umeona!
Suala la ndoa linahusisha "SISI " sio "MIMI",ukiwa bado singo ni wewe tu unajali ya kwako lakini ukishaolewa ni unapambana kumfurahisha mwenza wako ili wote muwe na amani.Kwahivyo ndoa inahitaji kujiandaa hasa na kuwa na utayari wa kushughulika na mtu wa ziada ukiachana na wewe mwenyewe kwahiyo jivunie sana maisha ya usingo uliyo nayo sasa.

Ukiwa singo unaamua kama leo ule au usile,utoke au usitoke ,upike au usipike ni suala la uamuzi wako lakini kwenye ndoa hayo yote ni lazima ufanye aidha Kwa maamuzi yako auKwa kulazimishwa na uwepo wa mwenza wako .

Achana na purukushani za kulazimisha ndoa na badala yake hakikisha unapambania ndoto,maono,wito wako na kuishi maisha ya kusudi.